

Maswali

1. Naamani alikuwa na shida gani?
2. Nani alimwambia Naamani vile anaweza kupona?
3. Nani alimpelekea mfalme wa Israeli barua?
4. Mfalme wa Israeli alifanya nini aliposoma barua?
5. Naamani alienda kuona nani amtibu?
6. Naamani alifikiria Elisha atamfanyia nini?
7. Ni ujumbe gani aliomtumia Naamani?
8. Nani alimsihi Naamani amtii nabii?
9. Nini ilifanyika kwa Naamani alipooga kwa Yordani?
10. Nabii Elisha alichukuwa zawadi yoyote kutoka kwa Naamani?

Majibu

1. Naamani alikuwa na ukoma
2. Msichana mtumwa aliambia Naamani vile anaweza kuponywa.
3. Mfalme wa Shamu alimtumia barua.
4. Mfalme aliuliza, "Mimi ni Mungu."
5. Naamani alienda kuona nabii Elisha.
6. Naamani alifikiria Elisha atatoka nje amuone.
7. Ujumbe wa Elisha ulitaka Naamani aoge kwa Yordani mara saba.
8. Watumishi walimsihi Naamani amtii nabii.
9. Naamani alipooga kwa Yordani alipona.
10. Elisha hakuchukua zawadi kutoka kwa Naamani.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 1



29 Naamani wa ukoma

Marejeo

2 Wafalme 5

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba lazima tumtii Mungu kwa namna anavyotuamrisha

Maneno maalum

1. Naamani + ukoma + Mfalme wa Shamu.
2. Mtumwa + Israeli + nabii anaponya
3. Mfalme wa Israeli + jemadari + barua
4. Elisha + farasi + magari + Naamani
5. Kasirika + watumishi + oga uwe safi
6. Yordani + osha + mara 7 + pona ngozi

29.1 Naamani alikuwa jemadari wa jeshi la Mfalme wa Shamu. Naamani alikuwa mtu wamaana sana, lakini alikuwa na ukoma. Alikuwa mgonjwa sana na alijua atakufa.

29.2 Wakati wa vita na Waisraeli, Naamani alirudi na msichana mdogo wa Israeli awe mtumishi wa mkewe. Huyu msichana alimuhurumia Naaman na akasema, “Kama Naamani angemwendea nabii wa Israeli, angemponya huu ukoma.”




Mkewe akamwambia Naamani alichambiwa na msichana. Naamani akaenda kumwambia Mfalme wa Shamu habari ya nabii.

29.3 Mfalme akasema, “Nitatumia mfalme wa Israeli barua.” Mfalme alimpea Naamani barua na dhahabu, fedha na mavasi apelekee nabii. Akamtuma kwa Mfalme wa Israeli. Naamani alimpa Mfalme wa Israeli barua na akasoma. “Nimemtuma jemadari wangu Naamani kwako,” barua ilieleza, “Umponye ukoma.” Mfalme wa Israeli hakuamini. Akasema, “Mimi ni Mungu wa kuuwa na kuhuisha, mbona ananitungia mtu wa ukoma nimponye? Anataka ukofi na mimi.”

29.4 Elisha alisikia maneno yenye mfalme alisema. Akamwambia, “Tuma Naamani kwangu. Atajua kwamba kuna nabii wa Mungu Israeli.” Naamani akaenda na farasi, magari na watumishi wake mpaka kwa nyumba ya nabii. Lakini Elisha hakutoka nje, badala yake alituma mjumbe. Mjumbe alimwambia, “Enda uoge kwa mto wa Jordani mara saba, na utapona ukoma.”

29.5 Naamani alikasirika sana. “Nilifikiri nabii atatoka nje aniombee na kunipungia mkono ili Bwana Mungu wake, aniponye ukoma,” akasema. “Je Abana na Farpari mito ya Shamu, si kubwa na nzuri kuliko mito ya Israeli?”



Akageusha gari lake na akaondoka kwa hasira, lakini watumishi wake wakamwambia, “Bwana wetu, kama nabii angekwambia kufanya jambo ngumu ungelifanya, tafadhali kubali aliyoyasema. Oga na uwe msafi.”

29.6 Naamani alipinduka na kuenda mpaka mto Yordani. Alijiosa maji ya mto Yordani mara saba, sawa na vile aliambiwa na nabii. Alipotoka majini, ngozi yake ilikuwa imepona na ikafanana na ya mtoto mdogo. Hakukuwa na ukoma tena.



Naamani alirudi kwa nabii Elisha akamshukuru. Akasema, “Sasa najua kwamba Mungu wa kweli duniani kote ni Mungu wa Israeli.” Alimpea nabii zawadi. Elisha alimkataza kwamba hakutaka zawadi kwa kufanya kazi ya Mungu. Naamani alipanda gari lake na kurudi Shamu akiwa mtu wa furaha sana.